
# Mtask – EAC – C2C (UUMBAJI MPAKA MASIHI)




Hii ndiye hadithi ya kweli kutoka yale maandiko ya Torati, Zaburi, na Injili.

## **1.** Adamu → Dhambi

Neno la Mungu linasema, kwamba hivyo mwanzo, Mungu aliumba kila kitu, na kilikuwa kizuri. Aliumba wanadamu kwa mfano wake na kuwaweka shambani. Mungu akamwambia Adamu, "Unaweza kuwa ya mti wo wote bustanini isipokuwa mmoja, ukila ya mti huu, kwa hakika, utakufa."
Siku moja, nyoka, ambaye alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote alifika kwa mwanamke na alimwuliza, "Je, Mungu amesema huwezi kula ya mti wo wote bustanini?" Na mwanamke alijibu, "Tunaweza kula ya mti wo wote isipokuwa mmoja, na tukigusa ama tukila kutoka huu, tutakufa." Nyoka akamwambia mwanamke, "Siyo kweli, Mungu anajua ukila ya mti huu utakuwa kama Mungu." Basi, mwanamke akaona na kutamani. Alishika na akala. Akampatia Adamu aliyekuwa pamoja naye. Mara moja, wakafumbuliwa macho na wakaona ya kwamba walikuwa uchi, na wakajificha na Mungu. Mungu akawatembelea bustanini, na akasema, "Adamu, uko wapi?" Adamu, akajibu, "Nimejificha kwa sababu niko uchi." Mungu akamwuliza, "Je, umefanya hivyo ndivyo nimekuambia usifanye?" Baada ya hivyo, Mungu akawahukumu na akawafukuza kutoka bustani. Uhusiano wao na Mungu ukaharibika kwa sababu wa dhambi yao.
Neno linasema ya kwamba dhambi iliendelea kuzidi duniani. Hata mtoto mmoja wa Adamu na Hawa akaua ndugu yake.

**2.** Ibrahimu → Imani

Baada ya muda, Mungu akaita mtu mwingine, kumwambia, “Toka nchi hii na uende mpaka nchi nitakuonyesha.” Ibrahimu akaenda mara moja. Alipofika, Mungu akamwambia wazawa wako watarithia nchi hii. Ibrahimu hakuwa na hata mwana mmoja. Mungu akamwambia ya kwamba kama huwezi kuhesabu nyota za mbingu, na tena mchanga wa bahari, itakuwa sawa na wazawa wake. Neno la Mungu linasema Ibrahimu akaamini na akahesabiwa haki. Mwishowe, Mungu akampatia mwana. Baada ya Ishmaeli (mtoto wake kutoka Hagar) kutoka nyumbani, Mungu akamwambia kumtoa mtoto wake mpendwa kama sadaka, na Neno linasema, akaenda mara moja. Walipofika mlimani, Ibrahimu akwaambia watumishi wake, “Kaeni hapa. Mimi na mwanangu tatamwabudu Mungu, na baada ya kumaliza, tutarudi.” Walipoenda, huyu mwana akauliza, “Baba, tuko na kuni, kisu, na moto, lakini mwana kondoo wa sadaka u wapi?” Ibrahimu akajibu, “Mungu atajipatia sadaka.”
Walipofika juu ya mlima, akamlaza huyu mwana, na alipoinua kisu kumchinja mwana, akasikia sauti kutoka mbinguni kusema, “Usimdarau mtoto wako. Sasa najua kweli uniamini.” Ibrahimu akaona kando na akaona kondoo akashikwa pembeni. Akatoa huyu kondoo kama sadaka ya kuteketezwa badala ya Isaka.
Neno la Mungu linasema bado wakazidi na dhambi badala ya kufuata ule mfano wa Ibrahimu.

**3.** Musa → Sheria (Njia ya Kumpendeza Mungu)

Baada ya miaka mingi, Mungu akamwita mwingine kuwaongoza wana wa Israeli. Mungu akamtumia kuwaondoa kutoka Misri, na kweli, Mungu akayatenda mambo mengi ya ajabu katika maisha yake. Kitu cha juu akafanya ni, katika safari yao kutoka Misri, Mungu akampatia Sheria katika Mlima wa Sinai. Juu ya kila kitu, akampatia Amri Kumi ambayo inasema, “Usiabudu miungu mingine, usiabudu masanamu, waheshimu mamako na babako, usiue, usiibe, usizine,” na kadhalika. Akaweka Sheria kama njia ya kumpendeza Mungu, lakini ilifika kweli kweli kama hukumu, kwa sababu hakuna aliye hai ambaye anaweza kutii kila kitu kila siku, basi ilikuwa lazima kutoa sadaka kwa ajili ya kuondoa dhambi.

**4.** Manabii → Utabiri Kuhusu Masihi

Neno linasema ya kwamba baada ya kupata Sheria, wengi wakasahau Sheria na wakawaabudu miungu mingine, na wengine, wakatii ama wakatenda Sheria, lakini wakasahau maana yake. Basi, baada ya miaka mingi, Mungu akatuma manabii wengi ambao wakafika kuleta ujumbe wa Mungu kuwahukumu watu, kuwaitia kurudi na wakasema “Kumtii Mungu ni mkuu kuliko kutoa sadaka,” yaani Mungu anasema matendo ya dini haitoshi kwake. Pia, hawa manabii wakatabiri kumhusu mtu ambaye atafika badaaye kuitwa Masihi. Wakatabiri kuhusu dalili zake, kama atazaliwa kutoka bikra (bikira), atazaliwa kutoka ukoo wa Daudi, na hata atazaliwa katika mji wa Daudi. Wakasema vitu vingi kuhusu maisha yake na ya umuhimu, wakasema huyu atateseka kama kondoo kuchinjwa kwa ajili ya dhambi za watu wote.

Basi, miaka mingi watu wakamngojea.

5. Yesu Masihi →Masihi Amefika (Utimizo wa Utabiri – Maisha na Huduma ya Yesu)

Baada ya miaka mingi, kulikuwa na bikra (bikira) akatembelewa na malaika ambaye akamwambia ya kwamba Mungu akamchukua kuzaa mwana kwa uwezo wake (siyo kwa mapenzi) na ya kwamba, jinsi atakapofika duniani, ataitwa Mwana wa Mungu. Kutoka ukoo wa Daudi, na hata akazaliwa mji wa Daudi, akafika duniani. Bado alipokuwa mtoto, wakuu wa Sheria wakastaajabu kwa sababu huyu akajua tayari Torati na Maandiko. Alipokuwa mzima, Yohana akamwona kusema, "Tazama Mwana Kondoo wa Mungu ambaye anaondoa dhambi za ulimwengu." Baadhi ya watu wakamfuata, na wengi wakastaajabu mafundisho wake. Akatuliza bahari na upepo, na wakajiuliza, "U nani?" Akaponya watu na kusamehe dhambi za watu, na wakajiuliza, "Huyu ni nani?" Akatoa mapepo, akafufua wafu, akaleta maoni kwa vipofu, na kuleta utembezi kwa wenye kupooza, na bado watu wakauliza, "Huyu ni nani?"
Akasema siku moja, "Kila amwaminiye [Masihi], asipotee, bali awe na uzima." Pia akatabiri kuhusu mateso yake.
Baada ya masiku kadhaa, viongozi vya Sheria wakamshika sirini na wakamhukumu kinyume wa Sheria, na mwishowe, Yesu akasulubishwa pamoja na wevi na mbele za washahidi, akafa, na kalafu akazikwa kaburini, na kaburi ikafungwa na maaskari. Siku ya tatu, wanawake ambao wakawa wanafunzi wake wakafika kaburini kuweka marashi mengine juu ya mwili wake, lakini wakaona hakuna mwili huko. Wanafunzi wengine wakaingia kaburi kuona sanda (shanda) huko, lakini hakuna mwili. Baada ya siku chache, akajionyesha mbele ya wanafunzi wake na washahidi zaidi ya mia tano. Baada ya siku arobaini, akapaa mbinguni.

Neno linatuambia ya kwamba Masihi akafika kwa sababu sisi sote tunatenda dhambi. Tumerithia uchafu wa dhambi kutoka Adamu na Hawa walipokataa kumtii Mungu na uhusiano wetu na Mungu ukaharibika. Katika Sheria, lazima lipo kwa dhambi zetu, lakini Mungu akapanga kitambo ya kwamba Masihi atafika kutoa pigo la dhambi tukiamini.